BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Ishirini na Tano – Tarehe 01 Juni, 2022

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka 2022/2023.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Uchumi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa Mwaka 2022/2023.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

116. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais,Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kwa kuwa Baraza la Mji wa Chake Chake limeamua kutumia Kware ya Makaani Vitongoji kama jaa kuu la Wilaya ya Chake Chake. Na kwa kuwa Kware hiyo ni muhimu kwa matumizi ya binadamu katika shughuli za kila siku za kimaisha zikiwemo kilimo, ufugaji, uchimbaji wa mawe, kifusi na kadhalika.

Na kwa kuwa uongozi wa Baraza la Mji Chake Chake hauko makini katika kuelekeza pamoja na kusimamia ulipaji wa taka hizo, jambo linalopelekea utupwaji holela na hupelekea kuzagaa kwa taka taka pamoja na kuenea kwa nzi ambao huzalisha magonjwa mbali mbali kama vile matumbo ya kuharisha damu.

(a) Je, Serikali inayo habari hiyo.

(b) Kama inayo, ni hatua gani zilizochukuliwa.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

82. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Nane ina dhamira ya kulipa madeni ya wanaotoa huduma katika Taasisi zake.

(a) Je, shughuli ya uhakiki wa madeni hayo imefikia wapi.

(b) Je, ni lini wadai hao wataanza kulipwa fedha zao.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

90. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Kwa kuwa Wizara iliahidi mbele ya Baraza hili kuyapima maeneo mbali mbali kwa lengo la kujulikana mipaka ya maeneo hayo na kuepusha migogoro ya ardhi baina ya wananchi.

Je, ni maeneo mangapi yamepimwa tangu kuingia madarakani Serikali ya Awamu ya Nane.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

130. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Ni jambo jema kwamba Serikali iliamua kununua meli mpya ya mafuta ili kutoa huduma stahiki za uingizaji mafuta Zanzibar sambamba na kuongeza ufanisi katika biashara ya meli na mafuta. Hata hivyo, kumekuwa na tuhuma kuhusu usahihi wa mpango huo.

(a) Je, meli mpya ya mafuta imenunuliwa kwa gharama gani na imekatiwa bima ipi.

(b) Je, tokea kununuliwa kwa meli hiyo imezalisha kiasi gani kama pato kwa Serikali.

(c) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kununua meli nyengine za biashara.

136. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Katika ujenzi wa barabara kongwe ya Wete-Chake iliahidiwa kwamba, kwa kadiri itakavyowezekana na kwa kadiri itakavyoonekana kuleta ufanisi, wafanyakazi na vibarua watatoka katika Mikoa husika ya Unguja na Pemba. Hata hivyo, imeripotiwa kwamba Kampuni ya MECCO inayoongoza ujenzi huo imekuwa ikiajiri wafanyakazi, vibarua na madereva kutoka nje ya visiwa vya Unguja na Pemba ambao ni wageni sana katika kisiwa cha Pemba hali ambayo inaweza kupunguza ufanisi.

(a) Je, Serikali inafahamu kwamba kuna madereva wameletwa na MECCO kutoka nje ya Zanzibar kwa ajili ya kazi za ujenzi wa barabara kongwe ya Wete-Chake.

(b) Je, ni upi muongozo wa Serikali kwenye ajira kama hizi zinazotokea katika kutekeleza miradi ya maendeleo katika Mikoa husika.

(c) Je, katika Mradi wa Ujenzi wa barabara kongwe ya Wete-Chake ni wafanyakazi wangapi wasio wataalamu wameajiriwa kutoka ndani na nje ya Mikoa husika.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

80. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeondoa suala la ugatuzi, na kwa kuwa sasa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ndio iliyopewa jukumu la kusimamia shughuli za elimu hapa nchini, na kwa kuwa tumeelezwa kwamba kuanzia mwaka huu wanafunzi wataanza kufanya mitihani ya darasa la saba badala ya darasa la sita kama ilivyokuwa awali, na kwa kuwa wanafunzi wa darasa la sita na darasa la saba wamekuwa wakisomeshwa mtaala sawa.

(a) Je, kwa nini wanafunzi wa madarasa hayo mawili kwa mwaka huu wa kwanza wasifanye mitihani kwa pamoja.

(b) Je, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imejipangaje kuhakikisha kwamba mtaala rasmi wa darasa la saba unapatikana kwa wakati.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka 2022/2023.



**Zanzibar,**
**01 Juni, 2022.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**